



Taarifa kwa vyombo vya habari  
Imezuiliwa hadi tarehe 4 Machi, 2014

## **Vurugu katika jamii hutokea kwa wingi zaidi kuliko wizi Lakini mara nyingi wananchi hawapati msaada wa polisi wanaouhitaji**

**Februari 19, 2014, Dar es Salaam:** Karibu nusu (46%) ya Watanzania wote wamearifu kuwa wameshawahi kushuhudia vurugu katika jamii katika kipindi cha miezi sita iliyopita, ikilinganishwa na idadi ya mtu 1 kati ya 5 (20%) anayeripoti kuwa amewahi kuibiwa kitu na wezi. Nusu (49%) ya Watanzania wote wanaripoti kuwa hawajawahi kuibiwa kitu na watu 4 kati ya 10 (37%) hawajawahi kushuhudia vurugu/ghasia katika jamii.

Matokeo haya yametolewa na Twaweza katika muhtasari wa utafiti wenye jina la *Je, Tuko Salama? Wananchi watoa taarifa kuhusu hali ya usalama wa nchi*. Muhtasari huu ni kwa mujibu wa takwimu kutoka *Sauti za Wananchi*, utafiti kwa njia ya simu za mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa uliofanyika kwenye kaya zote Tanzania Bara.

Wananchi wameripoti kuwa, kesi nyingi walizoshawahi kusikia zinazohusu mtu kutishiwa, kupigwa mawe au kuuawa, huwa ni makundi ya watu au watu binafsi wanaoyatenda na siyo polisi au jeshi. Kwa mfano, mwananchi 1 kati ya 5 (19%) ameshawahi kusikia habari za mtu kuuawa na kundi la watu, wakati ni wananchi 2 kati ya 50 (4%) tu walioshawahi kusikia mtu kuuawa na polisi. Hata hivyo, wananchi pia wamesema kuwa polisi mara nyingi huhusika anapokutwa mtu ametishwa, kupigwa au kupondwa mawe.

Wananchi wanapokumbana na uhalifu, wangependa kuripoti polisi, ingawa, ni nusu tu ya wananchi wote (47%) wanaofanya hivyo. Idadi ni kubwa katika maeneo ya mijini ambako watu 6 kati ya 10 (59%) waliripoti kuwa wangeweza kuripoti uhalifu polisi, ikilinganishwa na maeneo ya vijijini ambako watu 4 kati ya 10 (39%) ndiyo wangepanya hivyo. Hii inaweza kusababishwa na uwepo wa polisi kwenye maeneo ya mijini kuliko vijijini. Kitaifa, kwa mujibu wa maafisa watendaji wa vijiji na wenyekiti wa mitaa/vitongoji, jamii 6 kati ya 10 (62%) haina polisi. Maeneo ya mijini yana nafuu zaidi ambapo mitaa 4 kati ya 10 (36%) tu ndiyo yenye ukosefu wa polisi, wakati maeneo ya vijijini takriban vijiji 8 kati ya 10 (76%) waliripoti kutokuwa na maafisa wa polisi.

Walipoulizwa ni kwa nini watu hawaripoti uhalifu kwa polisi, Watanzania wamelaumu rushwa au polisi kutowahudumia ipasavyo wananchi. Mwananchi mmoja kati ya watano (22%) amesema kuwa atalazimika kumlipa polisi kiasi cha pesa ili apatiwe msaada, na idadi kama hiyo ya wananchi walisema kuwa polisi wasingewasikiliza au kuwajali wanapofikisha taarifa kituoni.

*Sauti za Wananchi* pia ilichunguza mtazamo wa watu kuhusu mfumo wa sheria. Kwa kawaida, watu wanaporipoti uhalifu kwa polisi, ni haki yao kutarajia kuwa polisi watajaribu kumkamata mhalifu na kisha kumfikisha mahakamani na hukumu kutolewa kwa mujibu wa sheria. Kwa ujumla, Watanzania wana imani ndogo kama haya yanatendeka. Nusu yao (52%) wanaamini kuwa kama mwananchi wa kawaida atafanya kosa/uhalifu, hataadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Jambo linalotia shaka, wananchi pia wana mtazamo wa kuwa kuna kukosekana kwa usawa mbele ya sheria kulingana na hadhi ya mtu: wananchi 7 kati ya 10 (67%) wanaamini kuwa mtu tajiri hawezi kuadhibiwa kwa uhalifu au kosa alilotenda, na wananchi 6 kati ya 10 wanaamini kuwa viongozi wa dini, maafisa wa polisi, viongozi waandamizi wa serikali na viongozi wa umma hawawezi kuadhibiwa kwa makosa/uhalifu wao.

*Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema "Kutokuwepo kwa imani na mfumo wa sheria pamoja na utumiaji wa njia zisizo rasmi ili kupata haki kuna dhoofisha usalama nchini. Upanuzi wa mifumo rasmi ya usalama na kuipatia sekta ya usalama rasilimali za kutosha ni sehemu ya ufumbuzi wa tatizo hili, ila bado hali inahitaji ubunifu zaidi na kufikiri kwa mapana. Masuala haya yanahitaji mjadala mkubwa wa umma, ikiwa ni pamoja na kwenye michakato ya Bunge la Katiba."*

---- Mwisho ----

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**

Risha Chande

Meneja Mawasiliano, Twaweza

**Baruapepe:** [rchande@twaweza.org](mailto:rchande@twaweza.org) | **Simu:** (+255) (0) 656 657559

#### **Maelezo kwa Wahariri**

- Muhtasari huu na takwimu zilizomo zinapatikana hapa [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org), au [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti)
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayomlenga raia na inayokusudia kuleta mabadiliko makubwa Afrika Mashariki. Twaweza inaamaini kuwa mabadiliko ya kudumu hayana budi kuanzia chini kwenda juu. Tumedhamiria kujenga mazingira na kupanua fursa ambazo zitatoa mwanya kwa mamilioni ya watu kuhabarishwa and kuwawezesha kuweza kuleta maendeleo katika jamii zao moja kwa moja na kuifanya serikali iwajibike
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:  
**Tovuti:** [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org) **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza\_NiSisi